# DARASA LA NNE - MWAKA 2016
# KISWAHILI

*1. Tumia penseli ya kawaida*

**MUDA: SAA MOJA DAKIKA AROBAINE**

*2. Hakikisha ya kwamba umeandika yafuatayo katika karatasi ya majibu:*
*(i) JINA LAKO (ii) JINA LA SHULE LAKO*

*3. Kwa kila jibu lako lionyeshe katika karatasi ya majibu na wala siyo katika hii ya maswali.*

***Soma kifungu kifuatavyo kisha ujibu maswali.***

Nyumba__1__ilikuwa karibu na kisima___2___ maji. Mvua___3___iliponyesha___4___walikorora sana.Tulichoshwa na mayowe___5__.Jambo__6___lilikuwa ni mbu__7__wakati___8___masika . Baada ya miezi___9___tulihamia nyumba___10___nzuri zaidi.

mwanafunzi huweka vitabu___11___dawatani. katika shule___12___kila darasa huwa na ___13___la kuweka vitabu. mbele ya darasa huwa na ___14___wa kuandika. Nyuma ya darasa letu kupandwa miti___15

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 1. | A. letu | B. chetu | C. yetu | D. mwetu |
| 2. | A. ya | B. cha | C. wa | D. la |
| 3. | A. mwingi | B. mingi | C. mengi | D. nyingi |
| 4. | A. machura | B. viura | C. vyura | D. chura |
| 5. | A.zao | B. yao | C. wao | D. chao |
| 6. | A. lingine | B. jingine | C.nyingine | D. ingine |
| 7. | A. wengi | B.nyingi | C. mingi | D. mengi |
| 8. | A. ya | B. wa | C. la | D. za |
| 9. | A. mbili | B. mawili | C. miwili | D. pili |
| 10. | A.zingine | B. ingine | C.nyingine | D. kingine |
| 11. | A. zake | B. vyake | C. yake | D. chake |
| 12. | A. kwetu | B. yetu | C. letu | D. mwetu |
| 13. | A. kabati | B. rafu | C. mkoba | D. viti |
| 14. | A. kalamu | B. kitabu | C. ubao | D. umbao |
| 15. | A. mengi | B. nyingi | C. zingi | D. mingi |

***Chagua kiashiria kifaacho katika swali la 16 - 17***

16. Jibu la pole dada! ni________
A. niko B. poa
C. nimeshapoa D. mzuri

17. Sisi kwetu tunakuna nazi tukitumia________
A. kinu B. mbuzi
C. chano D. uteo

***Jaza pengo kwa kiulizi sahihi***

18. Mwalimu________ananiita?
A. wepi B. mgani
C. yupi D. ngapi

19. Tupande miti________?
A. migani B. mingapi
C. upi D. yapi

***Andika kwa wingi***

20. Tunda hili ni bichi
A. Tunda hizi ni mbichi B. matunda hizi ni mbichi
C. Matunda haya ni mabichi D. Matunda haya ni mbichi

21. Amebeba kitabu changu
A. Wamebeba vitabu vyangu
B. Wamebeba vitabu vyangu
C. Wamebeba vitabu zetu
D. Wamebeba vitabu zangu

22. Taja umbo hili



A. duara
B. kasuku
C. mchduara
D. mchemraba

***Jaza pengo***

23. Birika________litapasuka
A. hii B. hizi
C. hicho D.hili

24. Samaki________wanaliwa
A. hawa B. hizo
C. huyu D. hii

25. Ni mnyama yupi anayefanana na ngo'mbe lakini ni mkali kuliko ngo'mbe
A. nyati B. ngiri
C. kifaru D. ndovu

***Andika katika wakati "Hu"***

26. Tumbombele alienda shuleni mapema
A. Tumbombele ameenda shuleni mapema
B. Tumbombele huendaga shuleni mapema
C. Tumbombele ataenda shuleni mapema
D. Tumbombele huenda shuleni mapema

***Kanusha***

27. Sisi tulikula viazi
A. Sisi hatukukula viazi
B. Sisi hatujakula viazi
C. Sisi hatuli viazi
D. Sisi hatukula viazi

28. Mama alipokuwa mgonjwa, alidungwa________
A. sidano B. sindano
C. shindano D. shidano

29. Kuwaongeza ngo'mbe ili walime kwa njia inayotakitana ni________
A. kuwaswaga B. kuwachapa



Test compiled by Schools Net Kenya, Term 1, 2016 | Available online at www.schoolsnetkenya.com
Contact details: E-mail: infosnkenya@gmail.com | Mobile: 0711882227

C. kuwafyeka D. kuwanyunyiza

Tegua kitendawili

30. Nanywa supu nyama natupa

A. samaki B. muwa
C. maembe D. maziwa

**Soma taarifa hii kisha ujibu maswali 31-40**

SHULE YA MSINGI YA MWANGAZA.
S.L.P 467.
KITUI
03/02/2014

Kwa rafiki mpendwa Otoyo

Salamu tele, nzito za heri, furaha na buraha kutoka kwangu rafikiyo. Mambo shuleni mwetu ni shwari bila shari na ya kuridhisha.

madhumuni ya barua hii ni kukuomba tuende pamoja jijini Songambele kwa kaka yangu shule zitakapofungwa kwa likizo ya nusu muhula. Kakangu Ochdo ameniomba niende nisherehekee pamoja na familia yake siku ya kuzaliwa kwa kifungua mimba wao, Kadibo. Usiwe na wasiwasi kuhusu hela kwani kaka ataigharamia safari hiyo.

Wasalimie ndugu zako, wavyele na marafiki zako.. Nakutakia kila la heri katika masomo yako. Tuonane shule zifungwapo.

Ni mimi mpenzi wa moyo
Kotise Kadede

31. Ni nani aliendakiwa barua hii______
 A. Kotise B. Ochido
 C. Otoyo D. Kadibo
32. Ni nani aliyeandika barua?
 A. Kaka B.Kadede
 C. Songambele D. Otoyo
33. mwandishi anasoma katika shule gani?
 A. Ya msingi B. Kitui
 C. Mwangaza D. Sogambele
34. Mwandishi alitaka rafikiye aende pamoja naye wapi?
 A. shuleni B. songambele
 C. mwangaza D. kitui
35. Hela za kusafiri huitwa_______
 A. nauli B. karo
 C. mahari D. kodi
36. mwandishi na rafikiye wangefunga safari yao wakati gani
 A. Likizo ya Aprili B. Likizo ya nusu mhula
 C. Likizo ya Desemba D. Likizo ya Agosti
37. Kulikuwa na sherehe gani?
 A. kuzaliwa kwa mwana B. krismas
 C. mwaka mpya D. mashujaa
38. Mwandishi atamwitaje kadibo?
 A. kaka B. binamu
 C. mpwa D. mjukuu
39. Barua hii inamalizika kwa_______
 A. kwaheri B. salamu
 C. swali D. mjukuu
40. Barua hii iliandikwa lini?
 A. Februari B. Februari 2014
 C. Machi 02 D. Machi 03

***Soma hadithi hii kisha ujibu maswali 41-50***

Tumbo moto alikuwa mzee aliyeishi katika kijiji cha Bidii. Mzee huyo aliishi peke yake kwenye nyumba ya nyasi. Alikuwa mvivu, tumbo moto alikuwa mlafi. Alionekana akizurura kila siku kutoka nyumba moja hadi nyingine akitafuta mlo kutoka kwa wanakijiji. Watoto wa Bidii walimfanya mzaha kwa sababu ya tumbo lake kubwa kama kiriba.

Mzee huyo alikuwa mchafu na hakupenda kuoga. Nyumba yake ilijaa funza na wadudu wengine. Nguo zake zilinuka fee! Hakuna aliyetaka kumkaribisha. Siku moja alipatwa na ugonjwa wa kipindupindu. Alipelekwa hospitalini kwa matibabu. kwa bahati nzuri alipata nafuu na kuruhusiwa kwenda nyumbani. Daktari alimshauri kuzingatia usafi wa mwili mazingira na hata mavazi.

Tumbo moto alibadilika na kuanza kujifanyia kazi mwenyewe kwenye shamba lake. Alizingatia usafi na kufanya bidii. Watu wa Bidii hawakuamini mabadiliko ya tumbo moto. Alianza kupokea wageni wa kila nyumbani kwake.

41. Tumbo moto aliishi wapi?
 A. kijijini B. nyasini
 C. bidii D. nyumbani
42. Tumbo Moto alikuwa_______
 A. mvivu na mlafi B. mwenye bidii
 C. safi na mlafi D. mlafi na mwenye bidii
43. kwani nini Tumbo moto alizurura kutoka nyumba moja hadi nyingine?
 A. alitafuta kazi B. alialikwa na majirani
 C. alitafuta chakula D. alipenda kuzurura
44. Ni nani alimfanyia mzaha_______
 A. wazee B. watoto
 C. akina mama D. vijana
45. Nyumba ya tumbo moto ilijaa nini?
 A. funza na wadudu B. nguo
 C. chakula D. kuni
46. Tumbo moto alipatwa na ugonjwa upi?
 A. malale B. ukimwi
 C. malaria D. kipindupindu
47. Kwa nini Tumbo moto alipatwa na ugonjwa
 A. kula sana B. kuzurura sana
 C. kutozingatia usafi D. kuishi peke yake
48. Daktari alimshauri Tumbo moto kufanya nini?
 A. kulima shamba lake
 B. kujenga nyumba nzuri
 C. kuzingatia usafi
 D. kuacha kuzurura
49. Neno daktari limetumiwa katika hadithi lina maana sawa na
 A. mwalimu B. tibabu
 C. tabibu D. hospitali
50. Baada ya ushauri wa daktari. Tumbo Moto alifanya nini?
 A. Alibadilika na kupanga nyumba
 B. Aliwafukuza wageni
 C. Alibadilika na kuanza kufanya bidii
 D. Alikataa ushauri

Kiswahili darasa la nne

Test compiled by Schools Net Kenya, Term 1, 2016 | Available online at www.schoolsnetkenya.com
Contact details: E-mail: infosnkenya@gmail.com | Mobile: 0711882227